TANGAZO LA SERIKALI Na. 240 la tarehe 4/4/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 790 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kufuta na kuandika upya tafsiri ya msamiati "mifugo" kama ifuatavyo:

Sura ya 184

"mifugo" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo;".

Marekebisho ya kanuni ya 11

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 11 kwa kuongeza maneno "isipokuwa kwa kuzingatia kanuni za kilimo" mwishoni mwa aya (a).

Dodoma
12 Machi, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi- OR-TAMISEMI*